# JARIBIO LA MTIHANI WA EMBU

# DARASA LA NANE - MWAKA 2019

# KISWAHILI:LUGHA

**Muda: Saa 1 Dakika 40**

## SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa karatasi hii ya maswali na karatasi ya kujibia. Karatasi hii ina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika karatasi hii
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika karatasi hii ya maswali.

## JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo umeandika katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
9. Kwa kila swali 1 - 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi **A, B, C, D**. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano:**
**Katika karatasi ya maswali:**

**21.** Kiungo kinachosafisha damu mwilini huitwa

A. ini
B. moyo
C. figo
D. muundi

Jibu sahihi ni **C. (figo)**

**Katika karatasi ya majibu:**

**18.** [A] [B] [C] [D] **19.** [A] [B] [C] [D] **20.** [A] [B] [C] [D] **21.** [A] [B] [C] [D] **22.** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **19.** Kisanduku chenye herufi C ndicho kilichorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

*Mwanafunzi aangalie kuwa maswali yote kwenye kijitabu hiki yameigwa chapa.*

Com
E

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1-15. Katika kila nafasi, chagua jibu mwafaka.**

Usafiri katika nchi ____1____ za kiafrika ni tatizo sugu. ____2____ watu hutembea kwa muda mrefu kwa miguu kwa ____3____ usafiri wa haraka. ____4____ hupanda hata ngamia ili wapige hatua ____5____, ngamia hutumiwa kusafirisha ____6____ ya mizigo. Waliofanikiwa kujinunulia magari ____7____ kuyafanyia ukaratabi mara kwa mara. Aghalabu inawabidi wajinunulie vifaa vya kuundia magari vyaani ____8____

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | mingi | mengi | nyingi | mwingi |
| 2. | kati ya | baadhi ya | miongoni mwa | mojawapo wa |
| 3. | kuukosa | kuikosa | kuyakosa | kumkosa |
| 4. | wengine | vingine | mingine | pengine |
| 5. | maadamu | angalau | pia | laiti |
| 6. | shehena | chane | kipini | doti |
| 7. | yana budi | zina budi | wana budi | hawana budi |
| 8. | vibori | vipuri | vifusi | vipuza |

Jukumu ____9____ uhifadhi wa mazingira si la serikali pekee ____10____ pia ni la wanajamii. Wananchi kwa viongozi wanafaa kushirikiana ili kufanikisha suala hili kwani ____11____. Kwa kuwa mazingira ni uhai. Hatuwezi kamwe ____12____ wito wa ____13____. Miti ikikatwa shelabala huenda taifa likageuka kuwa ____14____. Huu basi utakuwa msiba wa kujitakia ____15____ hauna kilio.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 9. | la | ya | wa | mwa |
| 10. | mbali | bali | bora | lau |

11. A. kina na kinga ndipo moto uwakapo B. damu ni nzito kuliko maji
C. Mungu si athumani D. hasira hasara

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 12. | kuhimiza | kufikiria | kupuuza | kuzingatia |
| 13. | kuzilinda | kuyalinda | kuilinda | kuilinda |
| 14. | jangwa | msitu | chemchemi | konde |
| 15. | ambalo | ambayo | ambazo | ambao |

**Kutoka swali la 16 - 30, chagua jibu sahihi**

16. Chagua sentensi inayoonyesha wakati uliopita muda si mrefu
    A. Mwalimu hutufunza
    B. Mwalimu atatufunza
    C. Mwalimu alitufunza
    D. Mwalimu ametufunza

17. Chagua jibu ambalo si aina ya shairi
    A. tathnia B. tathlitha
    C. ukwapi D. ngonjera

18. Haraka, mwakani, mara nyingi ni mfano wa
    A. vielezi B. vitenzi
    C. vivumishi D. vihusishi

19. Chagua jozi inayoonyesha kitenzi kilichoundwa kutokana na kivumishi
    A. Pika - upishi
    B. Uvimilivu - vumilika
    C. Amini - mwaminifu
    D. Safi - safisha

20. Chagua neno lenye sauti ghuna pekee
    A. baba B. faa
    C. kaka D. choo

21. Chagua sentensi iliyo sahihi kisafuri
    A. Nywele yake imenyolewa
    B. Nyasi imekatwa
    C. Mitume yote imefika
    D. Mijomba walivuliwa jana

22. Sayari iliyo ndogo kuliko zote ni
    A. zeibaki B. mshatari
    C. zohali D. mirihi

23. Ni sentensi gani inayoonyesha **'KWA'** ya mahali au kihusishi
    A. Nyumbani kwake kunapendeza
    B. Watoto kwa walimu walifika shuleni
    C. Nitaenda kwa mjomba wangu
    D. mwana aliadhibiwa kwa utovu wa nidhamu

24. Andika kwa usemi wa taarifa "Nikisikiliza kwa makini nitafualu" Bora alisema
    A. Bora alisema "Nikisikiliza kwa makini nitafaulu"
    B. Bora alisema kuwa akisikiliza kwa makini atafaulu
    C. Bora alisema kuwa angesikiliza kwa makini atafaulu
    D. Bora alisema kuwa angesikiliza kwa makini angefaulu

25. Chagua sentensi iliyo na maelezo sahihi.
    A. Umbu ni jina wanaloitana wanaume walioa katika nyumba moja
    B. Buda pia huitwa shaibu
    C. Ajuza ni rafiki wa mwanamke
    D. Kijana ni kisawe cha mvulana

26. Ni sentensi gani iliyoakofishwa barabara?
    A. Nilienda sokoni nikanunua: ndizi, mkate na mboga.
    B. Mwalimu wetu wa kiswahili anaitwaje
    C. Je! utakuwa mwanafunzi mzuri?
    D. Lo! baba amepata ajali

27. $^{3}/_{5}$ kwa maneno ni
    A. tatu kwa tano
    B. khumusi tano
    C. khumusi tatu
    D. sudusi tatu

28. Neno **"mkekani"** lina silabi ngapi?
    A. Tatu B. Nne
    C. Saba D. Sita

29. **Kanusha:** Mtoto ambaye alisoma alifaulu
    A. Mtoto ambaye alisoma hakufaulu
    B. Mtoto ambaye hakusoma hakufaulu
    C. Mtoto asiyesoma hakufaulu
    D. Mtoto ambaye alisoma hajafaulu

30. Jogoo ni kwa kikwara kama vile ajuza ni kwa
    A. buda B. bikizee
    C. pora D. shoga

Soma habari ifuatavo kisha ujibu maswali 31-40

Mtoto anapozaliwa huwa mchanga kiwango cha kutojielewa. Akili yake huwa bado changa kiwango cha kutojimudu. Kila mara ajuacho ni kilio tu. Kilio chake huashiria mambo mengi yaki wemo njaa. Kuumwa, kuugua au kutaka kubadilishwa viwinda. Akili yake huwa kama karatasi nyeupe ambayo haijaandikiwa chochote. Huwa hakika hana habari kuhusu yanayoendelea duniani.

Jambo la kushangaza yaani la ibra ni kuwa mtoto huweza kumtambua mama yake mzazi pindi anapozaliwa. Hata hivyo. mtoto huwa hana mwao iwapo anachopewa ni kizuri au kibaya. Almradi yeye hufurahia tu kile anachopewa na kudhani kuwa kinafaa.

Baada ya siku kadhaa, mtoto huweza kujau na kuanza kutambua watu vizuri. Mtu wa kwanza kutambuliwa ni mama yake. Wakati huo yeye huwa bubu anayefurahi na kucheka bila sababu yoyote. Mtoto ana uwezo wa kuchekea hata makosa.

Anapofika umri wa miezi sita, mtoto huanza kupewa uji, maziwa na vyakula vinono. Mtoto hulishwa kwa kijiko baada ya kufungwa kimori ili nguo yake isichafuke. Mama huhakikisha kuwa chakula cha mwana we ni laini ili kisimsakame.

Aghalabu mtoto hujifunza kutokana na mama. Mama bila shaka huwa ni mwalimu wa kwanza wa mtoto. Mtoto humpapasa mamaye mzazi kwenye mashavu akahisi ulaini wa ngozi yake. Huiga chochote anachokifanya mama. Wakati huo akili yake huanza kunakili mambo machache. Huanza kujifunza. Basi huo ndio ukuaji wa mtoto. Jambo hili na hatua hizi huhitaji uangalifu mkubwa sana ili mtoto huyu awe mwadilifu. Mama naye anafaa kuwa kielelezo chema ili mwana ayaige yafaayo, ama kweli, mtoto hutazama kisogo cha nina.

31. Kwa nini mtoto hawezi kujitegeema katika maisha yake ya mwanzo kwa mujibu wa aya ya kwanza?
A. Huwa dhaifu
B. Akili yake huwa safi
C. Akili yake huwa changa
D. Huhitaji msaada wa mama yake

32. Mtoto huwezaje kutambua mama?
A. Kwa kuyatazama mavazi yake
B. Kutumia hisia za maumbile
C. Hujua anavyocheka
D. Kupitia kilio chake

33. Gani kati ya haya hayawezi kumfanya mtoto kulia?
A. Njaa
B. Maradhi
C. Akiwa ameenda haja
D. Akibebwa na mama

34. Mwandishi amesema kuwa akili ya mtoto huwa kama karatasi nyeupe ina maana?
A. Akili yake huwa nyeupe
B. Huwa hana maarifa yoyote
C. Huwa ana maarifa mengi ya akili
D. Huwa mtoto mzuri sana

35. Kulingana na makala haya mwandishi anasema kuwa mwalimu wa kwanza wa mtoto huwa?
A. Mwalimu wa chekechea
B. Baba mzazi
C. Yaya wa mtoto
D. Mama mzazi

36. Kulingana na mwandishi ni neno gani la mwanzo ambalo mtoto huanza kujifunza?
A. Karatasi nyeupe
B. Uji
C. Maziwa matamu
D. Mama

37. Mtoto huwa hana mwao' sentensi hii imetumia tamadhali gani ya usemi?
A. Tashbihi
B. Nahau
C. Istiara
D. Methali

38. Mtoto anapozaliwa kwa kawaida
A. huwa mchanga kiasi cha kujielewa
B. hupenda kulia na kulala peke yake
C. huwa mchanga mwenye akili nyingi
D. huwa mchanga kiwango cha kutojielewa

39. Mtoto akilelewa vyema aghalabu huibuka kuwa mwema. Ni methali gani inayoweza kuthibitisha ukweli huu?
A. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu
B. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo
C. Kinga na kinga ndipo moto uwakapo
D. Mtoto akililia wembe mpe

40. Kichwa mwafaka cha habari hii ni?
A. Hatua za kuboresha kwa mtoto
B. Akili ya mtoto
C. Hatua za kukua kwa mtoto
D. Upendo wa mama na mtoto

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali41-50**

Bwana Tegemea alikuwa amekuzwa katika mazingira nyingi.Wavyele wake waliamini kuwa mtu akifunzwa kazi mapema, atakuwa mkakamavu maishani. Kwake Tegemea alichukulia kinyume kimoyomoyo alijiapia kuwa akipata kazi na aoe, kisha apate watoto hatawasumbua. Shuleni, alitia bidii akaipita mitihani yake ya viwango vya juu. Hatimaye. alienda ughaibuni kuyaongezea masomo yake.

Bado akiwa na dukuduku lile lake lahapo awali, aliziangalia familia za huko na kuvutiwa. Akayaona makuzi ya kwao kuwa yalikuwa ya kishamba. Akasahau kuwa kisomo cha kijadi alichopewa na wazazi kilikuwa ndicho chanzo cha ufanisi wake.

Baadaye alirudi kwao. akaoa na kujaliwa watoto wawili. Alimwambia mkewe kuwa, yeye hatathubutu kushikilia makuzi "ghushi" ya kizamani. Waama, alisahau kuwa mwacha mila ni mtovu. Hapo basi akawalea watoto wake kama mayai. Watoto walipoguswa kidogo. walishtakia hali kwa wavyele wao, nao waliwabwekea "wachokozi" kwa hasira na mabezo. Watu wakabakia macho tu! Watoto wakamea pembe za kinyati. Wakabaki kufanya lolote waliloliona katika runinga kwani hawakuwa na kazi yoyote ya kufanya. Waliropokwa ovyo popote pale bila ya tahayuri yoyote. Ngoma ikipigwa mno hupasuka kiwambo. Watoto wake walianza kulewa, kuvuta sigara na kutumia dawa za kulevya.

Vituko vilipozidi na kuvuka mipaka, walianza kuwadharau na kuwaaibisha wageni maskini waliowatembelea huko kwao waliowahi kufika kwao kwa vigari vya supana mikononi walichekwa. Hata watoto w'alishangaa walipoona watu wakipanda "matatu" au "mabasi walipokwenda kuchukuliwa shuleni kwa gari walilolipuuza. Tegemea na mkewe waliridhi matakwa ya watoto wao wakidhani kuwa huko kupenda. Walisahau kuwa kuna leo na kesho. Wakasikika wakisema, "watoto safi sana hawa. Ni jasiri na werevu. Hawana undani wowote" Wakasahau kuwa kuna yale yanayofaa kusemwa au kuna yale ya kumezea. Maneno mengine huchoma watu nyoyoni.

Watoto wa Tegemea walizidi kudidimia kisimani. Shule nayo ikawapiga chenga. Wakashindwamitihani yao ya kidato cha nne. Kama hali ya kuliokoa jahazi, wazazi wakawapa mitaji ya kuanzisha biashara. Hata hivyo, waliyafuja mali yote. Hatimaye ukata ukawanyemelea wakawa maskini hohehahe wasioweza kuwasaidia wazazi wao wazee. Walibaki kuhangaika lakini dunia haikuwaonea huruma. Tegemea na mkewe walijifunza kuwa mtoto <u>hakuzwi</u> kwa kubwagiwa mapesa na kuengaengwa. Anafaa kiifunzwa jinsi ya kuukabili ulimwengu bila ya kutegemea nundu za wazazi. Mtegemea cha nduguye hufa maskini.

41. Wazazi wa Tegemea

A. waliuwahi udongo ungali maji

B. hawakujali maslahi ya wana wao

C. walimpa Tegemea fursa ya kujiamulia

D. walikuwa watesi na wasumbufu

42. Tegemea alianza kuwa na mtazamo tofauti na makuzi yake

A. wakati alioa

B. wakati alipokuwa akiongeza masomo

C. wakati alipowapata watoto

D. wakati alipozaliwa

43. Ni mambo gani yanayoonyesha kuwa Tegemea ni mwachamila?

A. Kutopenda kazi nyingi, kwenda ng'ambo na kuvutiwa na huko

B. Kuvutiwana familia za ng'ambo. kupuuza makuzi yajadi

C. Kutowakaripia watoto kuwanunulia bidhaa ghali

D. Kuwapa watoto mitaji, kupuuza malezi ya jadi

44. Ughaibuni ni wapi?

A. Nchi za uzunguni

B. Nchi za masomo yajuu

C. Nchi zilizoendelea

D. Nchi za mbali

45. Mtazamo wa mwandishi ni kuwa

A. watoto wakilelewa bila maadali hupotoka

B. watoto wakipata elimu ya ju huwa wabaya

C. watoto waengeengwe na kupatiwa uhuru kufanya chochote

D. watoto wa kigeni ni bora kuliko wa kijadi

46. Tabia za watoto wa Tegemea si pamoja na

A. kulewa ovyo ovyo na kudharau watu

B. kuwasaidia watoto na kutia bidii masomoni

C. kuwadharau watu na kuzembea masomoni

D. kutia bidii na kuwabeza watu

47. Maana ya kuukabili ulimwengu bila ya kutegemea nundu kulingana na aya ya mwisho ni?

A. Mtu kuweza kujikimu bila kutarajia misada

B. Kulewa ovyoovyo

C. Kupambanana maisha kwa kuwategemea wengine

D. Kupiga dunia teke

48. Walipokwenda kuchukuliwa shuleni kwa gari walilolipuuza walijificha. Hii ina maana kuwa

A. walikuwa maskini sana

B. nyumbani kulikuwa na gari bora kuliko hilo

C. wapenda magari hayo ya supana mikononi

D. nyumbani kulikuwa na gari duni kuliko hilo

49. Kwa nini Tegemea alienda ughaibuni?

A. Ili aoe mke mzuri

B. Ili asionekane mshamba

C. Ili kuyaongeza masomo yake

D. Ili kuonyesha maringo yake

50. Ni nini kilichokuwa chanzo cha ufanisi wa Tegemea kwamujibu wa aya ya pili?

A. Kwenda ughaibuni

B. Kuzaliwa katika mazingira ya kazi nyingi

C. Kupata mitaji kutoka kwa wazazi

D. Kisomo cha jadi alichopewa na wazazi

E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com